

HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA

Simu Na 023 2402738
Fax Na. 023 - 2402706



S.L.P 10,
MKURANGA,
PWANI.

Kumb. Na. MDC/S.20/20/VOL. V/15

06 JULAI, 2021

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga anawatangazia watazania wote wenye sifa kuomba nafasi za kazi zifuatazo:

A. NAFASI ZA KAZI

MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III – NAFASI TANO (5).

B. NGAZI YA MSHAHARA

Waombaji wote watakaopata nafasi watalipwa mshahara katika ngazi ya mshahara ya TGS B.

C. MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIKI III

- 1) Afisa Masuhuli na Mtendaji mkuu wa Serikali ya kijiji
- 2) Kusimamia ulinzi wa usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika kijiji
- 3) Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kijiji
- 4) Katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- 5) Kutafsiri na kusimamia sera, sheria na taratibu
- 6) Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali
- 7) Kiongozi wa Wakuu wa vitengo vya kitalaamu katika kijiji.
- 8) Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji.
- 9) Mwenyekiti wa kikao cha watalaamu waliopo katika kijiji
- 10) Kupokea, kusilikiza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi
- 11) Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za kijiji
- 12) Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

D. SIFA ZA MWOMBAJI

1. Awe na Elimu ya Kidato cha Nne/sita.
Aliyehitimu mafunzo ya astashahada/cheti (**NTA LEVEL 5**) katika mojawapo ya Fani zifuatazo:
 - Utawala
 - Sheria
 - Elimu ya Jamii
 - Usimamizi wa Fedha
 - Maendeleo ya Jamii
 - Sayansi ya Sanaa kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.
2. Awe na umri usiopungua miaka kumi na nane (18) na usiozidi miaka arobaini na tano (45).
3. Awe amesajiliwa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) mwenye kadi au Namba ya Usajili wa NIDA

E. NAMNA YA KUTUMA MAOMBI:

Barua za maombi zikiwa zimeambatanishwa na Nakala ya vyeti vya Elimu na Taaluma zilizohibitishwa, Wasifu wa Muombaji (CV), picha mbili "Passport size" na namba za simu zitumwe kwa;

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya,
S.L.P 10,
MKURANGA.



MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI NI TAREHE 27/07/2021 SAA 9:30 ALASIRI.

Limetolewa na;

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya,
MKURANGA